06

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR, JUNI, MWAKA 2026

15 Julai 2026

## OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili; ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa Maeneo ya Utawala, kijiografia, na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi mbali mbali.


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumika na wapangaji, watunga sera, watoa maamuzi na wasimamizi wa sheria.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 27 zimeripotiwa mwezi Juni, 2026. Wilaya ya Kaskazini 'A' imeripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali nane (8) sawa na asilimia 29.6 ukilinganisha na wilaya nyingine.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Juni 2026**




Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Juni, 2026 zimepungua kwa asilimia 3.6 na kufikia ajali 27 kutoka ajali 28 zilizoripotiwa mwezi Mei 2026

Mwezi wa Juni 2026, Wilaya ya Kaskazini 'A' imeripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali nane (8) ikilinganishwa na wilaya ya Kati iliripotiwa kuwa na ajali sita (6) kwa mwezi wa Mei 2026.


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Juni 2026 na Mei 2026**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka zimeongezeka kwa asilimia 12.5 na kufikia ajali 27 kwa mwezi wa Juni 2026 ikilinganishwa na ajali 24 zilizoripotiwa mwezi wa Juni 2025.


Wilaya ya Kaskazini 'A' imeripotiwa kuwa na ajali zaidi kwa mwezi wa Juni 2026 (ajali 8) na wilaya hiyohiyo iliyoripotiwa kuwa na ajali zaidi mwezi Juni 2025 (ajali 4).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Juni 2026 na Juni 2025**




Jumla ya waathirika 51 wameripotiwa mwezi Juni, 2026 ambapo waathirika 38 walikuwa wanaume na waathirika 13 walikuwa wanawake (Kiambatanisho: Jadweli 3.4). Wilaya ya Kaskazini 'A' imeripotiwa kuwa na waathirika wengi, waathirika 13 sawa na asilimia 25.5 ikilinganishwa na wilaya nyengine.


**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Juni 2026**




Idadi ya waathirika waliofariki mwezi Juni 2026 imepungua kwa asilimia 5.0 na kufikia waathirika 19 kutoka waathirika 20 kwa mwezi wa Mei 2026.


Idadi kubwa ya waathirika waliofariki kwa mwezi wa Juni 2026 wameripotiwa kutoka wilaya ya Kaskazini 'A' ambapo wilaya ya kati imeripotiwa kuwa na idadi sawa ya waathirika kwa mwezi wa Mei 2026 (waathirika sita (6)) kwa kila wilaya.

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Juni 2026 na Mei 2026**





Idadi ya waathirika waliojeruhiwa mwezi Juni 2026 imeongezeka kwa asilimia 10.3 na kufikia waathirika 32 waliojeruhiwa mwezi Juni 2026 kutoka waathirika 29 walioripotiwa mwezi Mei 2026. Aidha, kwa mwezi Juni 2026, Wilaya ya Kati ilikuwa na idadi kubwa ya waathirika waliojeruhiwa (waathirika nane(8)) ikilinganishwa na Mwezi Juni 2026 idadi kubwa ya waathirika waliojeruhiwa waliripotiwa wilaya ya  Kaskazini 'B' (waathirika 9).

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi Juni 2026 na Juni 2026**




Waathirika waliofariki mwezi wa Juni 2026 wameongezeka kwa asilimia 11.8 na kufikia waathirika 19 kutoka waathirika 17 waliofariki mwezi wa Juni 2025. Idadi kubwa ya waathirika waliofariki kwa mwezi Juni 2026 wameripotiwa kutoka Wilaya ya Kaskazini 'A' waathirika sita (6) ikilinganishwa na mwezi Juni 2025 wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na waathirika wanne (4).

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Juni 2026 na Juni 2025**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwaka wameongezeka kwa asilimia 10.3 na kufikia waathirika 32 mwezi wa Juni 2026 ikilinganishwa na waathirika 29 mwezi Juni 2025. Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na waathirika wengi waliojeruhiwa kwa mwezi wa Juni 2026 (waathirika nane(8)) ikilinganishwa na mwezi Juni 2025 wilaya ya Kaskazini 'A' na Magharibi 'B' zimeripotiwa kuwa na waathirika sita (6) kwa kila wilaya.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Juni 2026 na Juni 2025**





Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani waliojeruhiwa na waliofariki mwezi Juni 2026, waathirika wengi (waathirika 29) walikuwa abiria, wakifuatiwa na wapanda baskeli na pikipiki 13, waendao kwa miguu nane (8) na dereva mwathirika mmoja (1).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Juni 2026**





Ajali nyingi zilizoripotiwa mwezi Juni 2026 zilitokea muda wa saa 12:01 hadi 03:00 asubuhi ambapo zimeripotiwa ajali nane (8).

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Juni 2026**




Kati ya ajali 27 zilizoripotiwa mwezi wa Mei 2026, ajali 17 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali 10 zimesababishwa na uzembe wa madereva. Mkoa wa Kaskazini Unguja umeongoza kuwa na ajali zilizosababishwa na kuendesha gari mwendo kasi (ajali 8). Mkoa wa Kusini Unguja na Mjini Magharibi imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya ajali zilizosababishwa na uzembe wa madereva (ajali 3 kwa kila wilaya).

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Juni 2026.**




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 8,883 yameripotiwa mwezi wa Juni 2026, ambapo makosa 8,877 yameripotiwa kwa wanaume na makosa sita (6) yameripotiwa kwa wanawake (Kiambatanisho: Jadweli 3.8).

Wilaya ya Kati ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani, makosa 1,612 sawa na asilimia 18.1 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa kwa mwezi Juni 2026. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa, makosa 60 (asilimia 0.7 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa).


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Juni 2026**




Kosa kuu lililoripotiwa mwezi wa Juni 2026 ni kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 2,548 yakifuatiwa na makosa ya kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 1,918) na kuendesha chombo cha moto bila ya leseni, bima na leseni ya njia (makosa 919).

Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya yote 10 yaliyoripotiwa mwezi Juni 2026 yamechangia asilimia 60.6.


**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani, Juni 2026**



Idadi ya makosa kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 14.7 na kufikia makosa 8,883 mwezi wa Juni 2026 kutoka makosa 10,408 mwezi wa Mei 2026.

Wilaya ya Kati imekuwa na idadi kubwa ya makosa ya barabarani kwa mwezi wa Juni 2026 (Makosa 1,612) ambapo pia wilaya hiyo iliripotiwa kuwa na idadi kubwa ya makosa kwa mwezi wa Mei 2026 (Makosa 2,182).


**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Juni 2026 na Mei 2026**




Idadi ya makosa kwa mwaka yameongezeka na kufikia makosa 8,883 mwezi wa Juni 2026 kutoka makosa 5,346 mwezi wa Juni 2025.

Wilaya ya Kati imekuwa na idadi kubwa ya makosa yaliyoripotiwa mwezi wa Juni 2026 (Makosa 1,612) na wilaya ya Mjini na Magharibi 'A' zilikuwa na idadi kubwa ya makosa yaliyoripotiwa mwezi wa Juni 2025 (makosa 908 kwa kila wilaya).

**Kielelezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Juni 2026 na Juni 2025**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi mbali mbali. Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabaraniza ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 27 zimeripotiwa mwezi Juni, 2026. Wilaya ya Kaskazini ‘A’ imeripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali 8 (6) sawa na asilimia 29.6 ukilinganisha na wilaya nyingine.

Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Juni, 2026 zimepungua kwa asilimia 3.6 na kufikia ajali 27 kutoka ajali 28 zilizoripotiwa mwezi Mei 2026. Mwezi wa Juni 2026, Wilaya ya Kaskazini ‘A’ imeripotiwa kuwa na ajali zaidi, ajali nane (8) ikilinganishwa na wilaya ya Kati iliripotiwa kuwa na ajali sita (6) kwa mwezi wa Mei 2026

Jumla ya makosa 8,883 yameripotiwa mwezi wa Juni 2026, ambapo makosa 8,877 yameripotiwa kwa wanaume na makosa sita (6) yameripotiwa kwa wanawake. Kosa kuu lililoripotiwa mwezi wa Juni 2026 ni makosa ya kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 2,548) sawa na asilimia 28.7 ya makosa yote yaliyoripotiwa.

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi ya Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa 2020-2026**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 51 | 19 | 19 | 18 | 22 | 8 | 33 |
| Februari | 44 | 25 | 16 | 13 | 19 | 6 | 36 |
| Machi | 21 | 18 | 21 | 13 | 14 | 20 | 31 |
| Aprili | 22 | 20 | 9 | 15 | 18 | 27 | 23 |
| Mei | 30 | 18 | 16 | 12 | 20 | 14 | 28 |
| Juni | 21 | 14 | 5 | 12 | 23 | 24 | 27 |
| Julai | 20 | 19 | 14 | 24 | 21 | 25 | |
| Agosti | 16 | 15 | 15 | 19 | 16 | 26 | |
| Septemba | 11 | 10 | 14 | 16 | 16 | 31 | |
| Oktoba | 23 | 19 | 11 | 16 | 19 | 31 | |
| Novemba | 21 | 20 | 20 | 14 | 21 | 20 | |
| Disemba | 26 | 12 | 12 | 21 | 13 | 28 | |
| **Jumla** | **306** | **209** | **172** | **193** | **222** | **260** | **178** |

**Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani walioripotiwa 2020-2026**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 89 | 44 | 36 | 38 | 40 | 10 | 43 |
| Februari | 76 | 40 | 29 | 19 | 49 | 8 | 47 |
| Machi | 40 | 31 | 60 | 16 | 27 | 48 | 44 |
| Aprili | 43 | 41 | 16 | 25 | 38 | 35 | 38 |
| Mei | 36 | 28 | 21 | 28 | 25 | 34 | 49 |
| Juni | 31 | 20 | 4 | 25 | 33 | 38 | 51 |
| Julai | 30 | 47 | 15 | 51 | 30 | 30 | |
| Agosti | 41 | 37 | 48 | 65 | 32 | 65 | |
| Septemba | 28 | 20 | 26 | 24 | 24 | 46 | |
| Oktoba | 60 | 71 | 17 | 25 | 36 | 51 | |
| Novemba | 44 | 45 | 28 | 26 | 54 | 32 | |
| Disemba | 34 | 20 | 23 | 43 | 25 | 37 | |
| **Jumla** | **552** | **444** | **323** | **385** | **413** | **441** | **272** |

**Jadweli 3.2: Idadi ya Waliofariki kwa Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa 2020-2026**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 24 | 11 | 19 | 15 | 13 | 8 | 24 |
| Februari | 20 | 13 | 16 | 11 | 23 | 8 | 22 |
| Machi | 13 | 17 | 14 | 12 | 8 | 21 | 19 |
| Aprili | 10 | 18 | 6 | 12 | 13 | 22 | 18 |
| Mei | 13 | 14 | 10 | 6 | 14 | 15 | 20 |
| Juni | 20 | 11 | 4 | 10 | 17 | 17 | 19 |
| Julai | 12 | 13 | 12 | 16 | 17 | 22 | |
| Agosti | 9 | 10 | 10 | 11 | 14 | 20 | |
| Septemba | 6 | 11 | 13 | 13 | 17 | 21 | |
| Oktoba | 16 | 21 | 8 | 14 | 16 | 32 | |
| Novemba | 17 | 16 | 14 | 12 | 24 | 15 | |
| Disemba | 20 | 13 | 10 | 21 | 13 | 21 | |
| **Jumla** | **180** | **168** | **136** | **153** | **189** | **222** | **122** |

**Jadweli 3.3: Idadi ya Waliojeruhiwa kwa Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa 2020-2026**

| Miezi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 65 | 33 | 17 | 23 | 27 | 2 | 19 |
| Februari | 56 | 27 | 13 | 8 | 26 | 0 | 25 |
| Machi | 27 | 14 | 46 | 4 | 19 | 27 | 25 |
| Aprili | 33 | 23 | 10 | 13 | 25 | 13 | 20 |
| Mei | 23 | 14 | 11 | 22 | 11 | 19 | 29 |
| Juni | 11 | 9 | 0 | 15 | 16 | 21 | 32 |
| Julai | 18 | 34 | 3 | 35 | 13 | 15 | |
| Agosti | 32 | 27 | 38 | 54 | 18 | 45 | |
| Septemba | 22 | 9 | 13 | 11 | 7 | 25 | |
| Oktoba | 44 | 50 | 9 | 11 | 20 | 19 | |
| Novemba | 27 | 29 | 14 | 14 | 30 | 17 | |
| Disemba | 14 | 7 | 13 | 22 | 12 | 16 | |
| **Jumla** | **372** | **276** | **187** | **232** | **224** | **219** | **150** |

**Jadweli 3.4: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Juni 2026.**

| Wilaya | Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla ya Wathirika | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Idadi | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 8 | 29.6 | 5 | 1 | 6 | 31.6 | 6 | 1 | 7 | 21.9 | 11 | 2 | 13 | 25.5 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 7.4 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 6.3 | 2 | 0 | 2 | 3.9 |
| Kati | 3 | 11.1 | 1 | 0 | 1 | 5.3 | 5 | 3 | 8 | 25.0 | 6 | 3 | 9 | 17.6 |
| Kusini | 2 | 7.4 | 2 | 1 | 3 | 15.8 | 2 | 4 | 6 | 18.8 | 4 | 5 | 9 | 17.6 |
| Mjini | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 7.4 | 1 | 0 | 1 | 5.3 | 3 | 0 | 3 | 9.4 | 4 | 0 | 4 | 7.8 |
| Magharibi 'B' | 3 | 11.1 | 0 | 1 | 1 | 5.3 | 4 | 0 | 4 | 12.5 | 4 | 1 | 5 | 9.8 |
| Wete | 2 | 7.4 | 2 | 0 | 2 | 10.5 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 3.9 |
| Micheweni | 1 | 3.7 | 1 | 0 | 1 | 5.3 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 2.0 |
| Chake chake | 3 | 11.1 | 2 | 1 | 3 | 15.8 | 1 | 1 | 2 | 6.3 | 3 | 2 | 5 | 9.8 |
| Mkoani | 1 | 3.7 | 1 | 0 | 1 | 5.3 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 2.0 |
| **Zanzibar** | **27** | **100** | **15** | **4** | **19** | **100** | **23** | **9** | **32** | **100** | **38** | **13** | **51** | **100** |

**Jadweli 3.5: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Juni 2026**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 4 | 5 | 1 | 6 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kati | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 3 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 4 | 5 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **27** | **1** | **0** | **1** | **0** | **0** | 0 | **3** | **2** | **5** | **16** | **8** | **24** | **6** | **1** | **7** | **5** | **1** | **6** | **5** | **1** | **6** | **2** | **0** | **2** |

### Jadweli 3.6: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi wa Juni 2026 na Mei 2026

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 | Mei-26 | Juni-26 |
| Kaskazini 'A' | 3 | 8 | 3 | 7 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 1 | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 2 | 9 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 3 | 1 | 8 | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |
| Kusini | 3 | 2 | 3 | 6 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 5 | 2 | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 2 | 3 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 3 | 4 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Micheweni | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Chake chake | 3 | 8 | 3 | 7 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 1 | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Mkoani | 4 | 2 | 9 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | 6 | 3 | 1 | 8 | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 |

**Jadweli 3.7: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi Juni 2026 na Juni  2025**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 8 | 6 | 7 | 2 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 | 4 | 6 | 1 | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 3 | 0 | 8 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Kusini | 1 | 2 | 1 | 6 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 5 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 3 | 2 | 1 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Magharibi 'B' | 3 | 3 | 6 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 1 | 2 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Micheweni | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Chake Chake | 2 | 3 | 2 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Zanzibar** | **24** | **27** | **21** | **32** | **17** | **19** | **0** | **0** | **1** | **1** | **12** | **24** | **6** | **5** | **7** | **6** | **6** | **7** | **2** | **2** | **4** | **6** |

**Jadweli 3.8: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Juni 2026**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 94 | 0 | 94 | 297 | 0 | 297 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 3 | 0 | 3 | 2 | 0 | 2 | 64 | 0 | 64 | 485 | 0 | 485 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 93 | 0 | 93 | 280 | 0 | 280 | 129 | 0 | 129 | 50 | 0 | 50 | 365 | 0 | 365 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 90 | 0 | 90 | 50 | 0 | 50 | 20 | 0 | 20 | 100 | 0 | 100 | 200 | 0 | 200 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 270 | 0 | 270 | 89 | 0 | 89 | 196 | 0 | 196 | 350 | 0 | 350 | 137 | 0 | 137 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 61 | 0 | 61 | 213 | 0 | 213 | 95 | 0 | 95 | 0 | 0 | 0 | 345 | 0 | 345 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 224 | 0 | 224 | 149 | 0 | 149 | 86 | 0 | 86 | 74 | 0 | 74 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 8 | 2 | 0 | 2 | 10 | 0 | 10 | 48 | 0 | 48 | 15 | 0 | 15 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 5 | 0 | 5 | 25 | 0 | 25 | 4 | 0 | 4 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 66 | 3 | 69 | 77 | 0 | 77 | 40 | 0 | 40 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 41 | 3 | 44 | 37 | 0 | 37 | 30 | 0 | 30 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **758** | **0** | **758** | **796** | **0** | **796** | **650** | **6** | **656** | **919** | **0** | **919** | **1918** | **0** | **1,918** |

**Inaendelea... Jadweli 3.8: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Juni 2026**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 0 | 15 | 520 | 0 | 520 | 20 | 0 | 20 | 951 | 0 | 951 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 68 | 0 | 68 | 730 | 0 | 730 | 11 | 0 | 11 | 1,366 | 0 | 1,366 |
| Kati | 100 | 0 | 100 | 55 | 0 | 55 | 200 | 0 | 200 | 160 | 0 | 160 | 180 | 0 | 180 | 1,612 | 0 | 1,612 |
| Kusini | 100 | 0 | 100 | 30 | 0 | 30 | 150 | 0 | 150 | 120 | 0 | 120 | 20 | 0 | 20 | 880 | 0 | 880 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 125 | 0 | 125 | 123 | 0 | 123 | 0 | 0 | 0 | 1,290 | 0 | 1,290 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 610 | 0 | 610 | 0 | 0 | 0 | 1,324 | 0 | 1,324 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 123 | 0 | 123 | 186 | 0 | 186 | 0 | 0 | 0 | 842 | 0 | 842 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 17 | 41 | 0 | 41 | 0 | 0 | 0 | 141 | 0 | 141 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 13 | 0 | 13 | 0 | 0 | 0 | 60 | 0 | 60 |
| Chake chake | 26 | 0 | 26 | 0 | 0 | 0 | 39 | 0 | 39 | 39 | 0 | 39 | 0 | 0 | 0 | 290 | 3 | 293 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 121 | 3 | 124 |
| **Zanzibar** | **226** | **0** | **226** | **85** | **0** | **85** | **746** | **0** | **746** | **2,548** | **0** | **2,548** | **231** | **0** | **231** | **8,877** | **6** | **8,883** |

Jadweli 3.9: Idadi ya Makosa Barabarani, Baina ya Mwezi wa Juni, 2026 na Mei, 2025

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha motobila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni,bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 4 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 90 | 94 | 304 | 297 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 7 | 2 | 54 | 64 | 383 | 485 |
| Kati | 0 | 0 | 120 | 93 | 150 | 280 | 52 | 129 | 220 | 50 | 450 | 365 |
| Kusini | 0 | 0 | 20 | 90 | 10 | 50 | 30 | 20 | 20 | 100 | 20 | 200 |
| Mjini | 0 | 0 | 350 | 270 | 0 | 89 | 510 | 196 | 205 | 350 | 362 | 137 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 61 | 13 | 213 | 250 | 95 | 569 | 0 | 320 | 345 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 224 | 0 | 149 | 121 | 86 | 214 | 74 | 561 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 12 | 8 | 17 | 2 | 15 | 10 | 46 | 48 | 25 | 15 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 10 | 20 | 5 | 67 | 25 | 35 | 4 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 45 | 69 | 64 | 77 | 53 | 40 |
| Mkoani | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 38 | 44 | 51 | 37 | 54 | 30 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **507** | **758** | **204** | **796** | **1088** | **656** | **1,600** | **919** | **2,567** | **1,918** |

Inaendelea... Jadweli 3.9: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni, 2026 na Mei, 2026

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za Serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 | Mei 2026 | Juni 2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 15 | 549 | 520 | 13 | 20 | 986 | 951 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 55 | 68 | 694 | 730 | 6 | 11 | 1199 | 1366 |
| Kati | 230 | 100 | 190 | 55 | 390 | 200 | 0 | 160 | 380 | 180 | 2182 | 1612 |
| Kusini | 10 | 100 | 0 | 30 | 0 | 150 | 5 | 120 | 5 | 20 | 120 | 880 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 198 | 125 | 129 | 123 | 0 | 0 | 1754 | 1290 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 328 | 0 | 426 | 610 | 0 | 0 | 1906 | 1324 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 102 | 123 | 376 | 186 | 0 | 0 | 1374 | 842 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 64 | 17 | 71 | 41 | 0 | 0 | 250 | 141 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 3 | 35 | 13 | 0 | 0 | 178 | 60 |
| Chake chake | 0 | 26 | 0 | 0 | 39 | 39 | 37 | 39 | 0 | 0 | 238 | 293 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 48 | 6 | 29 | 6 | 0 | 0 | 221 | 124 |
| **Zanzibar** | **240** | **226** | **190** | **85** | **1257** | **746** | **2,351** | **2,548** | **404** | **231** | **10,408** | **8,883** |

**Jadweli 3.10: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni 2026 na Juni 2025**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 2 | 0 | 42 | 94 | 183 | 297 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 26 | 2 | 224 | 64 | 0 | 485 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 93 | 0 | 280 | 10 | 129 | 363 | 50 | 130 | 365 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 90 | 20 | 50 | 10 | 20 | 10 | 100 | 260 | 200 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 270 | 0 | 89 | 0 | 196 | 80 | 350 | 143 | 137 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 61 | 0 | 213 | 55 | 95 | 133 | 0 | 214 | 345 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 224 | 0 | 149 | 0 | 86 | 63 | 74 | 92 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 3 | 8 | 0 | 2 | 11 | 10 | 60 | 48 | 29 | 15 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 5 | 5 | 23 | 25 | 10 | 4 |
| Chake chake | 0 | 0 | 2 | 3 | 17 | 0 | 15 | 69 | 23 | 77 | 0 | 40 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 14 | 44 | 25 | 37 | 14 | 30 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **5** | **758** | **37** | **796** | **148** | **656** | **1,046** | **919** | **1,075** | **1,918** |


**Inaendelea…Jadweli 3.10: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Juni 2026 na Juni 2025**

| Wilaya | Kushindwa kuandika Anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za Serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chomboza Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 | Juni 2025 | Juni 2026 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 15 | 347 | 520 | 3 | 20 | 599 | 951 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 43 | 68 | 395 | 730 | 2 | 11 | 690 | 1366 |
| Kati | 0 | 100 | 36 | 55 | 0 | 200 | 0 | 160 | 36 | 180 | 575 | 1612 |
| Kusini | 0 | 100 | 0 | 30 | 100 | 150 | 15 | 120 | 0 | 20 | 415 | 880 |
| Mjini | 230 | 0 | 0 | 0 | 90 | 125 | 365 | 123 | 0 | 0 | 908 | 1290 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 80 | 0 | 426 | 610 | 0 | 0 | 908 | 1324 |
| Magharibi 'B' | 180 | 0 | 0 | 0 | 70 | 123 | 445 | 186 | 0 | 0 | 850 | 842 |
| Wete | 22 | 0 | 0 | 0 | 25 | 17 | 0 | 41 | 26 | 0 | 176 | 141 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 3 | 11 | 13 | 0 | 0 | 54 | 60 |
| Chake chake | 0 | 26 | 0 | 0 | 31 | 39 | 11 | 39 | 0 | 0 | 99 | 293 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 6 | 9 | 6 | 0 | 0 | 72 | 124 |
| **Zanzibar** | **432** | **226** | **36** | **85** | **476** | **746** | **2,024** | **2,548** | **67** | **231** | **5,346** | **8,883** |


**Jadweli 3.11: Tozo Zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya Kesi, Juni 2026**

| Wilaya | Idadi ya Kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 951 | 37,287,950 |
| Kaskazini 'B' | 1,366 | 31,360,500 |
| Kati | 1,611 | 46,000,000 |
| Kusini | 881 | 40,436,500 |
| Mjini | 1,290 | 41,719,000 |
| Magharibi 'A' | 1,324 | 43,637,750 |
| Magharibi 'B' | 842 | 34,638,100 |
| Wete | 139 | 2,115,000 |
| Micheweni | 61 | 900,500 |
| Chake chake | 293 | 4,825,100 |
| Mkoani | 126 | 2,068,000 |
| **Zanzibar** | **8,884** | **284,988,400** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani Zilizoripotiwa kwa Wilaya, Juni, 2026**



**Kielelezo 2:Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya Juni, 2026**



## Zingatia Maelezo

Ajali za barabarani ni ajali yeyote iliotokea barabarani inayohusisha angalau chombo kimoja (chenye maringi mawili, matatu au manne). Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar)

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumiagari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu.Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**


**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
**MMP, Zanzibar**